

(20). Bahlul Aulizwa Swali

Siku moja Bahlul alikwenda katika Baraza la Harun Rashid na akaketi mbele yake. Kwa hayo, Harun aliudhika mno na alitaka amuaibishe Bahlul mbele ya wote waliokuwapo hapo. Alimwuliza: "Je Bahlul yu hadhiri? Nataka jibu la fumbo langu."

Bahlul alisema: "Ni lazima kwanza uniambie sharti lako na utoe ahadi ya kutonigeuka katika kutimiza ahadi hiyo."

Kwa hayo, Harun alisema: "Iwapo utanijulisha jawabu papo hapo basi nitakupa *Ashrafi* elfu moja na iwapo utashindwa kunijibu basi nitatoa amri ya kunyolewa kwa ndevu na masharubu yako, kisha utembezewe katika mitaa na vichocho vya Baghdad kwa kuaibishwa na kudhalilishwa."

Bahlul alimjibu "Ah! Mimi sijali wala sihitaji hizo *Ashrafi zako*, bali ninalo sharti moja iwapo nitaweza kulijibu fumbo lako."

Hapo Harun akasema: "Je sharti lipi hilo?"

"Iwapo nitaweza kukujibu basi nitataka uwatolee amri inzi wasinisumbue" alisema Bahlul.

Harun alifikiri kwa kitambo, kisha akasema: Hili jambo haliwezekani kwani inzi sio katika utii wangu."

Kwa hayo Bahlul aliangusha kichekesho na kwa mshangao akasema: Je kunaweza kutegemewa nini kutoka mtu ambaye hawezi hata kudhibiti kitu kidogo mno kama inzi?"

Kwa hayo, Bahlul aliwaacha wote katika hali ya mshangao. Kwa majibu hayo, uso wa Harun ulianguka na Bahlul alipoyaona hayo, alisema: "Nipo tayari kujibu swali lako bila sharti lolote."

Basi Harun alijikaza, na kuuliza: "Je ni mti upi ule ambao umri wake ni mwaka mmoja na unao matawi kumi na mawili na majani thelathini ni siku ambazo sehemu moja ni usiku na wa pili ni mchana."

Harun alistajabishwa kwa majibu. Na wote waliokuwapo pia walifurahishwa mno kwa busara ya Bahlul.

Source URL: <https://www.al-islam.org/node/24483>